**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKETI MOROGORO**

**MAOMBI YA MAREJEO NO. 35 YA 2020**

**BAINA YA**

**SALUM SHABANI KULUNGE & MWENZAKE 3 ........................WALETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ULUGURU PHARMACEUTICAL &**

**ASSOCIATES CO. LTD............................................................MJIBU MAOMBI**

**Tarehe: 21/05/2021**

Akidi: Mhe. A. E. Mwipopo, J

Mleta Maombi: Bw. Bilary Msaka, PR toka CHODAWU, kwa niaba ya Waleta Maombi.

- Waleta Maombi – Wapo.

Mjibu Maombi: Bw. Ignas Punge, Wakili, kwa niaba ya Mjibu Maombi

- Meneja wa Operesheni wa Mjibu Maombi yupo Mahakamani.

Karani: Neema

**Bw. Ignas Punge - Wakili:**

Naomba pingamizi la awali ambalo nilileta Mahakamani tarehe 21/07/2020 lisikilizwe kwa kuwa maombi haya ya Marejeo yameletwa nje ya muda. Amri ya Mahakamani ya tarehe 01/07/2020 ilieleza kuwa Mleta Maombi awasilishe Shauri jipya la Maombi kufikia tarehe 02/07/2020 lakini aliwasilisha shauri hilo tarehe 03/07/2020 kinyume na amri hiyo ya Mahakama. Amri za Mahakama inatakiwa zifuatwe hasa pale zinapotolewa kama Mahakama hii ilivyoeleza katika kesi ya **Mimutie Moikan Mollel dhidi ya The Mwalimu Nyerere Memorial Academy,** Maombi Na. 96

ya 2020, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi na kesi ya **Micky Gilead Ndetura dhidi ya Exim Bank (T) Ltd,** kesi ya Biashara Na. 4 ya 2014, Mahakama Kuu, Divisheni ya Biashara iliyoketi Arusha. Hivyo, naomba shauri hili lifutwe (struck out) kwa kuwa Mahakama haina Mamlaka ya kulisikiliza.

**Bw. Bilary Msaka - Mwakilishi Binafsi:**

Ni kweli kuwa tulitakiwa kuleta shauri hili tarehe 02/07/2020 lakini siku hiyo nilikuwa na kesi hapa Mahakamani. Hivyo nilishindwa kuwasilisha kesi hiyo tarehe 02/07/2020 na nikawasilisha tarehe 03/07/2020. Kwa kuwa jambo hilo lilikuwa ni nje ya uwezo wangu naomba Mahakama ione namna ya kutusikiliza.

**Mahakama:** Kama walivyoeleza pande zote mbili, mnamo tarehe 01/07/2020 Mahakama hii ilifuta (strike out) Shauri la Marejeo Na. 17 la 2020 baina ya Waadawa hawa kutokana na mapungufu ya shauri hilo lakini ikawapa kibali Waleta Maombi kufungua shauri jipya kufikia tarehe 02/07/2020. Hata hivyo, Waleta Maombi waliwasilisha shauri jipya la marejeo ambalo ni Maombi haya yaliyopo mbele yangu tarehe 03/07/2020. Sababu ya kuchelewa ni kuwa siku ya tarehe 02/07/2020 mwakilishi binafsi wa waleta maombi alikuwa na shauri jingine Mahakamani.

Ni maoni yangu kuwa pale kunapokuwa na amri ya Mahakama ya Mdaawa kuwasilisha au kufanya jambo fulani, jambo hilo hutakiwa kufanywa kama amri ya Mahakama inavyoelekeza. Kushindwa kutekeleza amri ya Mahakama kwa wakati kunafanya jambo hilo liwe batili kama

ilivyoelezwa katika kesi ya **Micky Gilead Ndetura dhidi ya Exim Bank (T) Ltd** na kesi **Mimutie Moikan Mollel dhidi ya The Mwalimu Nyerere Memorial Academy** ambazo zilinukuliwa na Wakili wa Mjibu Maombi.

Katika Shauri hili, amri ya Mahakama ni waleta Maombi kuwasilisha shauri jipya kufikia tarehe 02/07/2020. Lakini waleta maombi walifungua shauri hili tarehe 03/07/2020 na hivyo shauri kuwa nje ya muda. Kwa sababu hiyo, Mahakamani hii haina Mamlaka ya kusikiliza shauri hili kwa kuwa limefunguliwa nje ya muda. Hivyo nalifuta (strike out) shauri hili kwa Mahakama kukosa Mamlaka ya kulisikiliza.

A. E. Mwipopo

**JAJI**

21/05/2021